

Waliokwenda nchini India kupasuliwa moyo warejea

Na Joseph Mwendapole

WAGONJWA 14 wa moyo wengi wao wakiwa watoto waliokuwa India kwa upasuaji wa moyo wamereja nchini wakiwa na afya njema baada ya upasuaji.

Waliwasili jana jioni katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambapo walipokelewa na viongozi mbalimbali wa Klabu ya Lions ya Dar es Salaam (host).

Mratibu wa magonjwa ya moyo katika klabu ya Lions ya Dar es Salaam, Lion Dk. Rajni Kanabar, alisema wagonjwa hao walitibiwa katika hospitali ya Fortis Escorts iliyoko New Delhi, India.

Aliwashukuru wasamaria wema waliojitolea kusaidia wagonjwa hao akiwemo mfanyabiashara maarufu Mustafa Sabodo aliyetoa dola 20,000 na Wizara ya Afya ya Zanzibar kwa kufadhili watoto 15.

Alimshukuru pia Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Reginald Mengi ambaye amekuwa mfadhili wa muda mrefu kwa wagonjwa wa moyo wanaokwenda India kutibiwa moyo na Mbunge wa Hanang (CCM), Dk. Mary Nagu.

Alisema wagonjwa hao wali-fanyiwa upasuaji kwa gharama ya

dola 2,000 kila mmoja katika hospitali hiyo ya Fortis kiwango ambacho ni kidogo kulinganisha na hospitali nyingine duniani.

Alisema kati ya wagonjwa hao, yumo mtoto wa miezi sita, Baraka Rwegasira, ambaye alikuwa katika hali mbaya na alipelekwa hospitali ni hapo kwa gari la kubebea wagonjwa.

Alisema mtoto huyo alikuwa na matundu mawili kwenye moyo wake na alikuwa na maji hali ambayo ilimsababishia kukua kwa shida.

“Alipofika tu alipelekwa moja kwa moja hospitali na gari maalum la wagonjwa na kisha kuondolewa yale maji haraka na kisha upasuaji wenye mafanikio makubwa na sasa anaendelea vizuri,” alisema na kuongeza kuwa kuna mtoto mwingine wa miezi minne, Zulekha Issa, ambaye alikuwa na matatizo yanayofanana na hayo.

Mwenyekiti wa Lions Klabu ya Dar es Salaam host, Frank Goyayi, aliwaomba wasamaria wema kunde-delea kutoa michango ya hali na mali kufanikisha matibabu ya wagonjwa wa moyo.

Alisema wengi wa wagonjwa hao wamekuwa wakifa kwa kukosa matibabu ya hali ya juu ambayo wanashindwa kumudu kutokana na

PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE



Baadhi ya viongozi wa Klabu ya Lions ya Dar es Salaam (host), wakimpa mtoto Consolata Boniface, zawadi ya ua baada ya kurejea nchini kutoka India alikopelekwa kutibiwa ugonjwa wa moyo. Kutoka kushoto ni Rajni Kanabar, Frank Goyayi na Shiraz Rashid. Hafla ya kuwapokea watoto hao ilifanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana.

gharama kubwa.

“Tutambue kuwa kungekuwa na hospitali kubwa ya uhakika ya moyo

hapa hawa wagonjwa wasingekufa na ukiwasaidia dola 2,000 wakafanyiwa upasuaji umewekeza

kwenye maisha ya watu wa Tanzania ambao watakuwa na manufaa kwa taifa,” alisema Goyayi.